

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**



MKUU WA MKOA WA NJOMBE

SIMU: 026- 2790001

FAX: 026- 2790001

OFISI YA MKUU WA WILAYA,
S.L.P 02,
LUDEWA.

JUNI 12, 2022

TAARIFA KWA UMMA

Kamati ya Bunge ya kudumu ya Miundombinu sambamba na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Godfrey Kasekenya Jana Juni 11, 2022 wamepokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mheshimiwa Andrea Tsere pamoja na viongozi wengine wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa akiwemo Mbunge wa Jimbo la Ludewa Mheshimiwa Joseph Kamonga.

Pamoja na mambo mengine kamati hiyo ilifanya ukaguzi wa ujenzi wa barabara ya Zege inayo endelea na ujenzi ikiwa ipo hatua za mwisho ya kutoka Lusitu hadi Mawengi yenyenye urefu wa kilomota 50 inayo tarajiwa kukabithiwa tarehe 31/08/2022.

Aidha Kamati hiyo ikiambatana na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ilikagua barabara inayo tarajiwa kuanza rasmi kwa ujenzi tarehe 13/06/2022 na Mkandarasi wa Kampuni ya China Engineering anapaswa kuanza ujenzi wa barabara hiyo yenyenye urefu wa kilomota 50 na anapaswa kukamilisha ujenzi huo ndani ya muda wa Miezi 28, na barabara hiyo ya Itoni- Lusitu inajengwa kwa gharama ya Shilingi Bilioni 95 ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan tayari ametoa fedha hiyo.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Chrispin B. Kalinga".

**Chrispin B. Kalinga
Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini
Halmashauri (W) Ludewa**